

UTANGULIZI:

Chuo cha ADVENTIST WOMEN MINISTRY – VTC ni Chuo kinacho milikiwa na Kanisa la Waadventista wa Sabato Jimbo la Nyanza Kusini kikiwa chini ya Idara ya Huduma za Wanawake. Chuo hiki kiko katika eneo la ofisi za Jimbo, mkabala na Chuo cha Mali Asili barabara iendayo Airport ni kilometer 7 kutoka Mwanza mjini.

SHUKRANI:

Tunapenda kumshukuru Mungu kwa wema, ulinzi na Mapenzi yake anayotutendea tangu tulipo anza Mwaka 2016 – 2022 tunapofika kutoa taarifa ya kazi yake aliyotuitia kuifanya, jina la Bwana litukuzwe.

MIPANGO KAZI 2016 – 2022:

1. Kusajili Chuo
2. Kuongeza Wanafunzi
3. Kuongeza Fani
4. Kuongeza Madarasa ya kusomea Wanafunzi
5. Kupanua eneo la kuhamishia Chuo.

MAFANIKIO KATIKA UTEKELEZAJI:

1. USAJILI WA CHUO:

Chuo cha Adventist Women Ministry – VTC chenye usajili wa kudumu kwa sasa wenye namba NO. VET/MZA/FR/2020/C/098. Kina Fani Nne (4) zilizo sajiliwa.

VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY

Serial No: 00141

VETA

Certificate No: VET/MZA/FR/2020/C/098

Certificate of Full Registration

It is hereby certified that

ADVENTIST WOMEN MINISTRY VTC

situated at **KITANGIRI** Ward **ILEMELA (U)** District **MWANZA** Region

having satisfied the requirements for full Registration as a Vocational Training centre pursuant to VET Act Cap 82 RE. 2006 in category **C** on the **23rd** day of **JUNE, 2020**

after accreditation of the following program (s) leading to National Vocation Awards.

Occupation	Level
1. Design Sewing and Clothing Technology	II
2. Food Production	III

This certificate is valid up to **22nd** day of JUNE, 2025

Signature

Signature

VET Head Office

3

Picha 1: Nakala ya Cheti cha usajili wa kudumu wa chuo cha AWMVTC

FANI ZINAZO FUNDISHWA:

- I) Ushonaji
- II) Food Production (Hospitality & Tourism)
- III) Secretarial Full Course & Short Course NABE
- IV) Computer Application.



Picha 2: Baadhi ya fani zitolewazo katika chuo chetu cha AWM-VTC.

WATUMISHI WA CHUO:

Watumishi	Idadi
Mkuu wa Chuo	1
Mhazini	1
Academic	1
Mshauri wa Wanafunzi wa kike (Matron)	1
Walimu	6
Jumla	10

WANAFUNZI KUANZIA 2016 – 2022: IDADI YAO KWA MWAKA NA KWA FANI ZAO.

NO	MWAKA	IDADI	KOZI NDEFU	KOZI FUPI
1	2016	19	5	14
2	2017	32	24	8
3	2018	31	23	8
4	2019	29	17	12
5	2020	26	15	11
6	2021	25	12	13
7	2022	32	11	11
JUMLA		194	107	87

MATOKEO YA MITIHANI YA SERIKALI VETA KUANZIA 2016 – 2021

Mwaka 2021

FANI	LEVEL			CERTIFICATION/REMARKS					
	I	II	III						
Clothing & Textile (Ushonaji)	1	-	-	VC1	-	VC2	-	VC3	-
Secretarial and Computer	-	1	1	VC1	1	VC2	-	VC3	1
Food Production (Upishi na Uzalishaji Chakula)	-	-	-	-	-	-	-	-	-
JUMLA	1	1	1		1		-		1

Mwaka 2020

FANI	LEVEL			CERTIFICATION/REMARKS					
	I	II	III						
Clothing & Textile (Ushonaji)	2	3	-	VC1	2	VC2	1	VC3	-
Secretarial and Computer	3	4	-	VC1	4	-	-	-	-
Food Production (Upishi na Uzalishaji Chakula)	-	-	1	VC1	1	-	-	-	-
JUMLA	5	7	1		7		1		

Mwaka 2019

FANI	LEVEL			CERTIFICATION/REMARKS					
	I	II	III						
Clothing & Textile (Ushonaji)	3	-	-	VC1	-	VC2	-	VC3	-
Secretarial and Computer	8	-	-	-	-	-	-	-	-
Food Production (Upishi na Uzalishaji Chakula)	-	3	-	-	-	-	-	-	-
JUMLA	11	3					-		

Mwaka 2018

FANI	LEVEL			CERTIFICATION/REMARKS					
	I	II	III						
Clothing & Textile (Ushonaji)	10	-	-	VC1	-	VC2	-	VC3	-
Secretarial and Computer	-	-	1	VC1	-	VC2	-	VC3	1
Food Production (Upishi na Uzalishaji Chakula)	1	2	2	VC1	2	-	-	-	-
JUMLA	11	2	3	-	2	-	-	-	1

Mwaka 2017

FANI	LEVEL			CERTIFICATION/REMARKS					
	I	II	III						
Clothing & Textile (Ushonaji)	-	3	-	VC1	1	VC2	-	VC3	-
Secretarial and Computer	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Food Production (Upishi na Uzalishaji Chakula)	1	-	2	VC1	2	VC2	-	VC3	-
JUMLA	1	3	2	-	3	-	-	-	-

Mwaka 2016

FANI	LEVEL			CERTIFICATION/REMARKS					
	I	II	III						
Clothing & Textile (Ushonaji)	2	-	-	VC1	-	-	-	-	-

MAFUNZO YANAYO TOLEWA YANAWAFAIDISHA WALENGWA KAMA IFUATAVYO:

Mafunzo ya ufundi yanayotolewa wengi yana wafaidisha kwa njia zifuatazo:

- Wengi sana wanajiajili na kuajili wengine, pia wana wafundisha wengine kwenye garment zao.
- Wengine baadhi wanaendelea na masomo ya juu hadi kufikia viwango vya Diploma za Mafunzo ya ufundi, wengine wanafikia kuwa Walimu wa Vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi. Hivyo wanapata ajira za kudumu maishani mwao. Na pia wanakuwa msaada kwa familia zao na watu wa kutegemewa na jamii.
- Kwa kupitia Neno la Mungu wanalo jifunza wakiwa hapa Chuoni wengine wanamuona Bwana na kumpokea kama Bwana na Mwokozi wa maisha yao Milele, ndio maana wanabatizwa.

UINJILISTI:

Chuo cha Adventist Women Ministry – VTC, Chuo kama kituo cha (TMI) Uinjilist kwa muda wa miaka 7 sasa tumebatiza Wanafunzi kama ifuatavyo:

a) Jedwali

MWAKA	WALIO BATIZWA	WA KIKE	WA KIUME
2016	6	6	-
2017	3	3	-
2018	5	4	1
2019	3	3	-
2020	4	4	-
2021	2	2	-
2022	3	3	-
JUMLA	26	25	1

b) Matunda ya ubatizo kwa wanafunzi hawa:

Mmoja kati yao alipomaliza masomo yake alipofika nyumbani kwao aliwashuhudia imani ya ki-Adventista katika familia yao na kuongoa watu wa tano (5) akiwemo mama yake mzazi, dada zake wawili (2), wifi yake na kaka yake jumla 5 yeye wa sita (6) kwa sasa familia hiyo ni Waadventista wa Sabato.

Mwongofu mpya huyu alipata kazi na sasa anaendelea na kazi kama Meneja wa Hotel. Mwongofu mpya huyu alifanikiwa kuwa mwadilifu na kufunga ndoa na Mungu amembariki kupata Watoto Wawili (2).

Pia Vijana wengi wa kike wanaosoma katika Chuo hiki kimekuwa kama sehemu ya kisima kwao, wengi wamefanikiwa kupata Wachumba aidha Wachungaji, Walimu Wafanyabiashara, wanaajiriwa, wanafunga ndoa zao, na wanaendelea na maisha yao vizuri wakiwa na ujuzi ulio sheheni. Kati yao wanasema “sijuti kuja kusoma Chuo cha Adventist VTC maana nimepata Mbaraka wa haja ya Moyo wangu”.

MWISHO:

Nina waomba na kuwasihi Chuo Cha AWM VTC ni kama kituo cha Elimu ya ujuzi na Uinjilisti, tusaيدiane wote kuhimiza na kuleta Wanafunzi.

Asanteni Mungu awabariki sana.